

MAJARIBIO YA MTHANI DARASA LA SABA

MUHULA WA KWANZA-KISWAHILI-2019

1. Hakikisha umeandika

MUDA: SAA I DAK. 40

(i) Jina lako

(ii) Jina la shule yako

Soma kifungu kifuatacho. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.

1 usemi wangu, napenda 2 nyuma kidogo tuangalie hali ya dunia 3 siku hizi. Sisi tunafahamu kwamba mipango yoyote ile 4 inaweza kufanikiwa tu 5 kuna amani duniani. 6, sisi tumepeleka 7 wetu katika umoja wa 8 na nchi 9 ili kusaidia kuleta amani duniani. Tunashukuru kuona kwamba jambo hili limeleta 10 zaidi na kuondoa hofu ya vita vya silaha. Sababu kuu ya watu kuvaa ni 11 ingawa 12 sababu mbalimbali kama vile kujikinga na baridi, 13 utamaduni wake, kutambuliwa cheo chake 14 kule kutaka 15 watu.

- | | | | |
|------------------------|------------------|------------------|------------------|
| 1. A. Kabla sijamaliza | B. Baada ya | C. Mbele ya | D. Kabla ya |
| 2. A. tupinduke | B. turudi | C. tuwe | D. tupite |
| 3. A. mzima | B. zima | C. yote | D. nzima |
| 4. A. tunazozifanya | B. tunafanya | C. tunayoifanya | D. tunayoyafanya |
| 5. A. isipokuwa | B. maadamu | C. iwapo | D. ilhali |
| 6. A. Kwa hivyo basi | B. Kwa ajili hii | C. Licha ya hayo | D. Fauka ya hayo |
| 7. A. wajumbe | B. magavana | C. mabalazi | D. wageni |
| 8. A. madola | B. mataifa | C. bara | D. ulimwengu |
| 9. A. nyingineyo | B. nyingine | C. nyinginezo | D. nyingi |
| 10. A. uhasama | B. uelewano | C. makabiliano | D. utumwa |
| 11. A. kujisitiri | B. kujificha | C. kusifiwa | D. kusitiri |
| 12. A. ipo | B. yapo | C. ndiyo | D. zipo |
| 13. A. kuzorotesha | B. kuhifadhi | C. kubadilisha | D. kudunisha |
| 14. A. badala ya | B. mighairi ya | C. mbali na | D. zaidi ya |
| 15. A. kuvutia | B. kusifu | C. kubeza | D. kukera |

Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu swali

ukifuata maagizo uliyopewa.

- | | |
|--|---------------------------|
| 16. Tamko katika shairi ni _____
A. mshororo
C. kina | B. mizani
D. kibwagizo |
| 17. Kurunzi ilimulika _____
A. waa
C. mwa | B. muu
D. lika lika |
| 18. Ni lipi lisilo vazi la kike?
A. Masombo
C. Buibui | B. Bombo
D. Kaniki |
| 19. Kanusha sentensi ifuatayo:-
Amekula na amekunywa.
A. Hajakula na hajakunywa.
B. Hajala wala kunywa.
C. Hajala wala hajanywa.
D. Hajakula wala hajakunywa. | |

20. Chagua sentensi ambayo imetumia -ki- ya masharti.
- A. Mvua ilinyesha kwa kani tulipokuwa tukidurusu.
- B. Seneta atakuwa akisimamia miradi katika gatuzi.
- C. Wanafunzi wasipomakinika hawatafaulu katika mitihani.
- D. Marijali wengi hupenda kutembea kijeshi.
21. Maneno ambayo yana matamshi ambayo yamekaribia haitwa _____.
- A. vitate B. visawe
- C. vitawe D. viarifa
22. Mtu ambaye hufichua siri za nchi yake huitwa _____.
- A. msiri B. jasusi
- C. balozi D. msaliti
23. Ni methali gani yenye maana sawa na; "Mkono utoao ndio upatao"?
- A. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe
- B. Jino la pembe si dawa ya pengo
- C. Mkono mtupu haulambwi
- D. Jaza ya hisani ni hisani.
24. Kanusha:-
Kusoma
- A. Kuandika B. Usinome
- C. Kusomesha D. Kutosoma
25. Kati ya akisami hizi, ni ipi akisami tasa?
- A. $\frac{3}{6}$ B. $\frac{3}{12}$
- C. $\frac{1}{5}$ D. $\frac{12}{24}$
26. Nomino baharia liko katika ngeli gani?
- A. LI - YA B. U - ZI
- C. A - WA D. YA - YA
27. Wadudu waitwao mchwa huishi katika _____.
- A. zeriba B. kidurusi
- C. kombe D. kizimba
28. Hamisi ni babaye Rono na Cherop. Njeri ni mkewe Rono. Je, Hamisi atamwitaje Njeri?
- A. Mkemwenza
- B. Mwanyumba
- C. Wifi
- D. Mkazamwana
29. Waziri wa elimu alitupongeza kwa kutia fora katika masomo yetu. Yaani alitupa mkono wa _____.
- A. tanzia B. tahania
- C. Iddi D. buriani
30. Suleiman alitaka apishwe njia na wenzake. Alisema _____.
- A. niwie radhi B. samahani
- C. ebul D. simile!

Soma ufahamu ufuatao kwa makini kisha ujibu maswali 31 - 40.

Mara nyingi simba huitwa mfalme wa wanyama. Ni kweli simba ni mnyama anayetisha. Zifuatazo ni sababu zilizomfanya kuwa mnyama wa kutisha. Ana meno yawezayo kuvunja mifupa ya nyati, kucha ziwezazo kutatulia mbali nyama ya mnyama mwingine yeyote, kinywa kinachoweza kufunguka na kuingia kichwa cha mja, nguvu zinazomwezesha kuliruka boma huku amebeba kwa mdomo wake ng'ombe dume ambaye amemuua, mngurumo unaomtisha kila kiumbe na wepesi wa mbio ambao kwa masafa mafupi, unaweza kufikia kilomita tisini na sita kwa saa. Hakuna shaka kwamba simba anajulikana zaidi kuliko wanyama wote wa Afrika. Yeye ni mmojawapo wa jamii ya paka. Ikiwa umeshamwona simba bila shaka umeshaona jinsi afananavyo na paka mkubwa. Jamii ya paka ni jamii ya hayawani muhimu sana, na kuna aina mbalimbali za paka duniani zizizopungua hamsini. Simba ni mojawapo na walio wakubwa kupita paka wengine na kwa kawaida hufikiriwa kuwa ni mkuu wa paka wote. Kuna simba wengi sana barani Afrika. Simba

wachanga huzaliwa na madoadoa ngozini. Kwa kawaida, huzaliwa watatu pamoja au pengine huwa wawili tu na pengine huenda wakazaliwa hata sita pamoja. Simba jike anawapenda sana watoto wake na simba dume husaidia kuwalinda wanapokuwa wachanga.

- | | |
|---|---|
| <p>31. "Simba ni mnyama wa kutisha" kwa hivyo anajulikana kama _____.</p> <p>A. jamii ya paka</p> <p>B. mnyama mwenye nguvu</p> <p>C. mfalme wa wanyama</p> <p>D. mnyama mkubwa kuliko wote</p> <p>32. Jamii ya simba iko na idadi kama _____ hivi.</p> <p>A. ishirini B. arubaini</p> <p>C. hamsini D. thelathini</p> <p>33. Kinywa cha simba kukifunguliwa kinaweza kuingia _____.</p> <p>A. mwili wa binadamu B. kinywa cha mja</p> <p>C. kichwa cha adinasi D. ng'ombe mzima</p> <p>34. Simba akimua mnyama yeye humbeba kwa _____.</p> <p>A. miguu yake ya mbele</p> <p>B. mdomo wake</p> <p>C. mabega yake</p> <p>D. miguu yake ya nyuma</p> <p>35. Kucha za simba hutumiwa _____.</p> <p>A. kupigana na wanyama wengine</p> <p>B. kuratulia nyama ya wanyama wengine</p> <p>C. kuwachoma wanyama wenzake</p> <p>D. kujikinga na adui zake</p> | <p>36. Wepesi wake simba humwezesha _____.</p> <p>A. kuona mbali zaidi</p> <p>B. kujikinga kutokana na hasidi</p> <p>C. kupinduka kwa haraka</p> <p>D. kukimbiza windo lake</p> <p>37. Kwa kawaida, simba huwazaa shibli _____.</p> <p>A. wawili B. wanne</p> <p>C. watano D. watatu</p> <p>38. Meno ya simba humsaidiaje?</p> <p>A. Kula nyama pamoja na nyasi</p> <p>B. Kuvunjavunja mifupa ya wanyama</p> <p>C. Kutafuna nyama zilizooza</p> <p>D. Kufagia wanyama waliofia porini</p> <p>39. Simba wachanga huzaliwa wakiwa na _____.</p> <p>A. macho yasiyoona vizuri</p> <p>B. miguu isiyo na makucha</p> <p>C. madoadoa ngozini</p> <p>D. meno yasiyo makali</p> <p>40. Kazi ya simba dume ni kulinda jamii, naye simba jike ni _____.</p> <p>A. kuwatunza vikembe wake</p> <p>B. kuwasafisha viduchu kwa ulimi wake</p> <p>C. kuwaweka watoto katika pango lake</p> <p>D. kuwapeleka watoto mtoni wakanywe maji</p> |
|---|---|

Soma ufahamu ufuatao kwa makini kisha ujibu maswali 41 - 50.

Ama kwa hakika yasemwayo yapo, kama hayapo yaja. Siku ambayo tuliisubiri kwa hamu na ghamu ilifika. Ingawa tuliisubiri kwa muda mrefu mno, lakini tulivumilia. Naam, subira huvuta heri na mvumilivu hula mbivu.

Niliamka alfajiri na mapema kuliko siku hizo nyingine. Niliangalia huku na huko nione kama kweli kulipambazuka. Na hakika kama mauti, kulikuwa kumepambazuka kabisa. Na kote kulikuwa kweupe pepepe kama theluji. Niliondoka kuelekea bafuni kuoga haraka bila kujali kwamba pole pole ndio mwendo.

Nilioga kwa maji baridi kama barafu lakini sikujali. Nilikuwa na furaha riboribo kama kibogoyo aliyeota jino. Nilifurahia safari ya kwenda kuwaona waigizaji mashuhuri. Nilioga haraka na kutoka mbio kurudi

chumbani ili nikavali sare zangu. Lo! Katika harakati hizo nilianguka lakini sikuumia. Hapo ndipo nilipoamini dhahiri shahiri kuwa haraka haraka haina baraka. Baada ya kuvalia vizuri niliingia jikoni kufungua kinywa. Kifungua kinywa kilikuwa kitamu kama asali. Nilikunywa chai nzito kwa vipande vya viazi. Nilishiba. Baadaye niliondoka kuelekea shuleni. Nilikiona kila kitu ambacho nilikiona njiani. Nilifurahi moyoni. Kweli kipendacho moyo ni dawa.

Kule shuleni gari lilikuwa tayari likitusubiri. Tuliingia na kuketi ndani ya gari tukipiga domo. Tulifika katika jumba la burudani bila kutambua. Tuliwaona waigizaji tele. Walikuwa wengi kama nzige.

Nilifurahi kuwaona wakiigiza maonyesho mbalimbali na kuiga wahusika tofauti tofauti. Kilichonifurahisha sana ni aliyekuwa akiigiza nafasi ya twiga kwa urefu wake na shingo ndefu iliyobeba kichwa kidogo. Hakika wahenga hawakukosea waliposema, kutembea kwingi ndiko kuona mengi.

- | | |
|--|--|
| <p>41. Msemaji alitarajia kuelekea wapi?
A. Kutembelea mbugani
B. Kukimbia shuleni
C. Kusoma shuleni
D. Kuzuru vyumba vya burudani</p> <p>42. “Na hakika kama mauti” ni mfano wa _____.
A. tashihisi
B. tashbihi
C. istiaara
D. tasfida</p> <p>43. Kulingana na kifungu, ni kweli kusema kuwa mnenaji _____.
A. alianguka chini alipoenda kuoga
B. aliwahi kutembelea vyumba vya burudani
C. alianguka chini alipoenda kuvalia sare
D. alisindikizwa na wazaziwe hadi shuleni</p> <p>44. Methali ipi inaafikiana na “Mvumilivu hula mbivu”?
A. Mchumia juani hulia kivulini
B. Baniani mbaya kiatu chake dawa
C. Akili ni nywele kila mtu ana zake
D. Mchagua jembe si mkulima</p> <p>45. “..... nilikunywa chai nzito kwa vipande vya viazi.” Eleza matumizi haya ya <u>kwa</u>.
A. sababu
B. sehemu ya nzima
C. matumizi
D. pamoja na</p> | <p>46. Mwandishi anasema kuwa _____.
A. alichukizwa na ‘simba’ kwa ukubwa wake
B. aliridhishwa na ‘pundamilia’ kwa rangi yake
C. alichukizwa na ‘ndovu’ kwa pembe zake
D. aliridhishwa na ‘twiga’ kwa urefu wake</p> <p>47. tukipiga domo..... ni sawa na kusema _____.
A. tukisengenya
B. tukiiongea
C. tukiimba
D. tukipiga kamsa</p> <p>48. Chakula kipi huliwa wakati wa usiku?
A. Chajio
B. Kishuka
C. Staffahi
D. Kisebeho</p> <p>49. Dhamira kuu ya habari hii ni _____.
A. kuwahimiza wanafunzi wawe waigizaji
B. kuwahimiza wanafunzi kuamka alfajiri
C. kuwahimiza wanafunzi watembelee mbuga za wanyama
D. kuwahimiza wanafunzi kutetea wanyamapori</p> <p>50. Methali bora kwa habari hii ni _____.
A. Asante ya punda ni mateke
B. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani
C. Kutembea kwingi ni kuona mengi
D. Haraka haraka haina baraka</p> |
|--|--|